

**Ni Nini Kimetokea Katika  
Uaminifu Wa Wakristo Leo?**  
**(What Has Happened To Integrity Of  
Christians Today?)**

**Na**

**John Kombo**

**Ni Nini Kimetokea Katika  
Uaminifu Wa Wakristo Leo?  
(What Has Happened To Integrity Of  
Christians Today?)**

**Na**

**John Kombo**

**Novemba 10, 2014**

# Ni Nini Kimetokea Katika Uaminifu Wa Wakristo Leo?

Unapofanya maamzi kuhusu kuwa mkweli au mdanganyifu, mwema au kutokuwa mwaminifu, mwenye haki au asiye na haki, wanadamu mara nyingi huzingatia “kujiingiza” kwa wale wasio na uaminifu. Watakuwa wakweli endapo wakijisikia kuwa itakuwa ni faida kwao; lakini watakuwa haraka, na bila kusita, kuamua kutokuwa wakweli kama wakidhani gharama ya kuwa wakweli ni juu sana. Watu kama hao mara nyingi hawaaminiki, hawatabiriki, na hawana chembechembe za nidhamu. Huwezi kuwatarajia waseme ukweli isipokuwa wakiamini kuwa ilikuwa na faida kwao. Hivyo basi, hakuna awezaye kuamini kama wanasema ukweli kuhusu chochote.

Kwa sababu ya ubinafsi, masengenyo, na tamaa, idadi kubwa wakiacha uaminifu wamejiweka wenyewe katika maangamizi. *“Ukamilifu wao wenye haki utawaongoza. Bali ukaidi wao wenye fitina utwaangamiza.”* (Mit. 11:3).

Uaminifu hutafsiriwa kama “kanuni za tabia njema, ukweli uliokamilika na uimara pasipo kuwa na dhamira ya kuigiza.” Kinyume chake ni unafiki, uongo, na utapeli. Mtu akiwa mkweli, hajiweki katika udanganyifu au kuvaa sura ya bandia, tofauti naa ilivyo kuwa. Atakuwa mkweli zaidi na anayefaa kuaminiwa katika yote asemayo na kufanya, kama ilivyo pingwa kwa yule mdanganyifu au anaesingizia wengine. Hii inajumuisha uongo, wizi, kudanganya, au aaina yo yote ya uongo. Mfalme Daudi alimzungumzia mtu mwaminifu katika Zaburi 15:1-4: *“BWANA ni nani atakaye kaa katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake katika kilima chako kitakatifu? Ni mtu aendaye kwa ukaamilifu na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake, asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, wala hakumsengenya jirani yake. Machoni pake mtu asiyejaa hudharauliwa, bali huwaheshimu wamchao BWANA ingawa ameapa kwa hasara yake, hayabadili maneno yake.”*

Tunaweza kuishi kama Mwokozi wetu alivyoishi alipotembea katika ulimwengu huu. Alikuwa mkweli sana. Hakujaribu kuficha chochote, maana hakukuwa na chochote katika maisha yake ambalo angeonea aibu. Yesu hakumsema mtu uongo au kudanganya kwa mtu hata mmoja. Siyo tu kwamba aliishia katika maneno ya sarakasi, au aina yo yote ya uongo, kupotosha na kuchanganya au kufunika kile alichomanisha bali kila wakati aalisema ukweli pasipo kujali matokeo au madhara. Alikuwa mpenda watu, mkweli, mwenye haaki, na mwema kwa watu wote.

Hivyo uaminifu, mara zote ni gharamaa, iligharimu maaishaa ya Mwana wa Mungu.

Badala ya kunyoosha vidole vya lawama kwa wafanya kazi wenzetu katika shambaa la Bwana wetu, tujifunze kuwarekebisha wenzetu kwa kunyoosha vidole vyetu katika maandiko Matakatifu. Alafu maandiko Matakatifu itakuwa “...lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki,” (2 Tim. 3:16).

John Kombo

Nakuru, Kenya







